# Serikali kuimarisha sekta za uzalishaji

NA SALAMA MOHAMMED, WKUMM

**MRATIBU wa Mradi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi Tanzania, Miza Suleiman Khamis, amesema serikali zote mbili za Tanzania zitaendelea kuimarisha sekta za misitu, kilimo, maji na ardhi katika maeneo yaliyoharibiwa ili kuongeza uzalishaji, upatikanaji na usalama wa chakula.**

Akizungumza huko katika ukumbi wa Chuo kikuu cha taifa Zanzibar kampasi ya Maruhubi baada ya kufungua kikao cha utambulisho wa Mradi huo kwa wadau kutoka katika Taasisi mbali mbali za serikali na zisizo za kiserekali.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na wenyeviti wa Jumuiya za wakulima za wilaya ya Kaskazini Unguja, alisema mradi huo utashughulika na maeneo yaliyokatwa miti, kilimo pamoja na usimamizi wa vyanzo vya maji na mipango Miji.

Aidha Miza alifahamisha kuwa andiko la mradi huo limelenga kuimarisha mashirikiano makubwa baina ya wadau mbali mbali kwa ajili ya kutatua changamoto zilizomo katika maeneo yaliyoharibiwa ili yaweze kuimarishwa yaendelea na shughuli za kilimo pamoja na urejeshaji wa miti katika maeneo yaliyokatwa.

Mratibu huyo ambaye pia ni Afisa Misitu alisema mradi huo unalenga kuanzisha jukwaa jumuishi la kukuza usimamizi wa rasilimali ardhi, maji, urejeshaji wa mnyororo wa thamani wa Zao la Mpunga ili kuzuia ukataji wa miti na uharibifu wa ardhi.

Mapema Mshauri elekezi kutoka katika Mradi huo, Saleh Kombo Khiar alisema mradi huo utawawasaidia wananchi wa wilaya za Kaskazini ‘A’ na ‘B’ ambapo utaangalia zaidi maendeleo endelevu ya mandhari ya mkoa na kuandaa uwiano katika matumizi ya ardhi, maji na kurejesha msitu uliopotea.

Kwa Upande wake Mkuu wa Divisheni ya eka na ukaguzi kutoka Kamisheni ya Ardhi Zanzibar, Abdulnassir Fadhil Mzee, alieleza kuwa kamisheni imeweka mpango bora wa ardhi utakaonesha maeneo ya uhifadhi, biashara, utalii na kilimo.

Hivyo alieleza kuwa jamii inatakiwa kuwa tayari kufuata mipango itakayowekwa na serikali kupitia Halmashauri ili kutambua sehemu sahihi itakayokubalika kwa makaazi na shughuli nyengine.

Aliongeza kuwa kupitia jukwaa lililoundwa wataweza kutatua migogoro ya ardhi kwa kutoa wa elimu kwa Jamii, kuimarisha taasisi za serikali na taasisi binafsi ili kuendelea kuimarisha mkoa wa Kaskazini Unguja na kuleta maendeleo mazuri katika wilaya hizo.

Mradi huo unaotekelezwa katika wilaya za mkoa wa Kaskazini Unguja kwa upande wa Zanzibar unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) pamoja na Global Environment Fund ambapo Dola za Marekani 2,351,754 zinatarajiwa kutumika ndani ya wa miaka mitano.

## Madiwani Mjini watakiwa kuwa mabalozi wema baada ya utumishi

NA HAFSA GOLO

**MSTAHIKI Meya wa Baraza la Manispaa Mjini, Ali Haji Haji, amewataka Madiwani wawe raia wema na kusimamia sheria na taratibu za nchi baada ya kustaafu majukumu yao ya uongozi.**

Alitoa nasaha hizo wakati akizungumza na Madiwani wa Manispaa hiyo katika mkutano wa mwisho baraza hilo uliofanyika ukumbi wa manispaa, Darajani mjini Unguja.

Alisema katika kipindi chote watakachomaliza muda wao wa udiwani ni vyema wakaendelea kuwa mabalozi wa kuelimisha jamii juu ya maendeleo ya miradi iliyotekelezwa na serikali.

Aidha alisema ipo haja kwa madiwani hao kuendeleza tabia ya uaminifu,uadilifu na kuhakikisha wanatumia hekma na busara wakati wanapofanya shughuli zao.

“Haitopendeza kusikia miongoni mwenu yupo mtu anashajihisha vitendo viovu ama ametuhumiwa kwenye matendo mauvu nasema hivi maana huko nyuma yalijitokeza mambo kama hayo mstaafu diwani mwenzetu”, alisema.

Aidha alisema yapo mambo mengi mazuri ya maendeleo yaliotekelezwa na serikali ambayo yamesaidia kukuza uchumi na mengine yamo kwenye majimbo yenu baadhi ya madiwani hivyo ni vyema kuwaelezea wananchi.

Hata hivyo alisema,aliwapongeza kwa uwajibikaji, kuhoji baadhi ya changamoto zinapojitokeza pamoja na kudumisha mashirikiano baina yao na watendaji wa Baraza la Manispaa.

Naye Diwani wa wadi ya Kikwajuni, Khamis Fataki ‘Ngasa’, alisema yeye ni muongoni mwa viongozi walionufaika kwa ujenzi wa miradi ya maendeleo iliyojengwa na serikali jimboni kwake.

Alibainisha miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa maji safi na salama,kiwanja cha michezo na barabara.

Kwa upande wake Diwani wa wadi ya Migombani, Jacob Joseph Owera, aliahidi kutekeleza na kusimamia nasaha walizopatiwa na Meya huyo kwani kufanya hivyo kutasaidia kudumisha nidhamu na heshima ndani ya jamii.



*MAKAMU Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania, Zainab Khamis Shomari, akizungumza na viongozi wa ka ngazi ya Mikoa, Wilaya na Majimbo wa jumuiya hiyo katika Afisi Kuu ya CCM Zanzibar, Kisiwani Unguja. (NA MPIGA PICHA WETU).*

## Tushikamane CCM iendelee kushika dola - Shomari

NA MWANDISHI WETU

**MAKAMU Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania, Zainab Khamis Shomari, amewataka viongozi wa umoja huo kuwa na umoja na mshikamano utakaowezesha kufanya kazi kwa ufanisi.**

Shomari ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu (MNEC) ya CCM taifa, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa ka ngazi ya Mikoa, Wilaya na Majimbo katika Afisi Kuu ya CCM Zanzibar, Kisiwani Unguja.

Alieleza kuwa wakati huu chama hicho na nchi ikielekea kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika baadae mwaka huu, viongozi hao wanapaswa kuzidisha ushirikiano utakaokiwezesha chama hicho kupata ushindi wa kishindo na kuendelea kushika Dola.

Aidha aliwahimiza viongozi hao kutenda haki kwa kila Mgombea atakayewania nafasi za uongozi katika uchaguzi wa ndani ya chama wakati wa mchakato wa uchaguzi wa ndani utakapoanza ili kuepusha mgawanyiko wa chama.

Wakati huo huo, mwenyekiti huyo, leo anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika bonanza la UWT mkoa wa Mjini (kichama) itakayoambatana na ugawaji wa vifaa mbali mbali vikiwemo vya michezo utakaofanyika leo katika viwanja vya kumbu kumbu ya Mapinduzi, Muembe Kisonge Unguja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na umoja huo, pamoja na vifaa vya michezo, vifaa vyengine vitakavyokabidhiwa ni viti mwendo kwa watu wenye ulemavu na majiko ya gesi ya kupikia ambapo Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM taifa na umoja huo mkoa wa Mjini, Tabia Maulid Mwita atahudhuria.